



MALALAMIKO KUHUSU MALIPO KWA WALENGWA

Kitengo cha Habari na Mawasiliano cha TASAF kinapenda kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko ya walengwa waliofanya kazi katika miradi ya jamii na kucheleweshewa malipo yao. Aidha Kitengo kinatumia fursa hii kuelimisha jamii kuhusu miradi ya ajira za muda na kulipwa ujira. Miradi ya ajira ya muda ni utaratibu wa utekelezaji miradi ya jamii yenye kutumia nguvu kazi, inayoshirikisha walengwa kufanya kazi na kulipwa ujira. Utaratibu huu unafahamika kwa walengwa wote na kabla haujaanza kutekelezwa walengwa huitishwa mkutano na kupewa taarifa za taratibu za miradi hii na taratibu zake.

Miradi inayotekelezwa kupitia ajira za muda inabuniwa na walengwa wenyewe kwa kuangalia mapungufu na kero mbali mbali ambazo zinawakabili. Miradi inayoibuliwa na jamii iko ya aina mbali mbali lakini mingi inahusu upatikanaji wa maji, barabara za vijijini, malambo ya kunyweshea mifugo, hifadhi ya mazingira na masoko

Utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya ajira za muda ni kama ifuatavyo:

1. Walengwa wanaoruhusiwa kufanya kazi ni watu wenye umri kati ya miaka 18 hadi 65 wasio walemavu, wajawazito au wenye watoto wenye watoto wenye umri wa chini ya miaka miwili
2. Kazi hufanywa na mwakilishi wa kaya, au mwakilishi-mbadala wa kaya
3. Utekelezaji wa miradi ya nguvu kazi huchukua miezi 6. Kila mwezi mlengwa anafanya kazi kwa siku kumi tu
4. Muda wa kufanya kazi kwa siku ni saa nne. Wakati wa kazi, anakuwepo mtaalam mwelekezi kusimamia utendaji wa kazi
5. Malipo kwa kazi hufanyika kila baada ya miezi miwili ambapo mlengwa atalipwa ujira wa siku alizofanya kazi ambazo hazizidi siku 20 kwa kila kipindi cha miezi miwili ya malipo
6. Malipo ya walioshiriki utekelezaji hufanyika mara baada ya taarifa zao kuwasilishwa TASAF kwa ajili ya maandalizi ya malipo.

Kutokana na sababu za kiutendaji malipo ya walengwa yaliyokuwa yafanyike mwezi March 2023 hayakuweza kufanyika. Taarifa kuhusu kuchelewa kwa malipo ya walengwa zilitolewa kupitia mikutano ya vijiji, vipindi vya radio, televisheni na magazeti. Kuchelewa kwa malipo kulileta sintofahamu kubwa kwa walengwa wetu na kupelekea kutoa malalamiko yao kwenye vyombo vya habari. Kitengo cha Mawasiliano kinaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

Tunapenda kutoa taarifa kwamba malipo kwa walengwa yamefunguliwa kuanzia 05/6/2023 na yataendelea kulipwa hadi 19/6/2023 hivyo walengwa wote watalipwa stahili zao ndani ya kipindi hiki. Zoezi hili la malipo linaenda sambamba na kufanya tathmini ya hali za walengwa ili kuwaondoa wale ambao hali zao kiuchumi zimeimarika na hivyo kupoteza vigezo vya kuwemo kwenye Mpango. Kwa taarifa zaidi, tunapatikana kwa simu kwa namba za bure 0800 110057 na 0800 110058 ambazo ziko wazi Jumatatu mpaka Ijumaa kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 2.00 usiku.

Imetolewa na Kitengo cha Habari na Mawasiliano

TASAF